# MWINJILISTI

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  MWINJILISTI. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MHUBIRI

1.Mwinjilisti ?...........................................................

2. Kusudi la mwinjilisti................................................

3. Kanisa..............................................................

4. Wenye  dhambi (Mataifa)...................................

5. Wokovu...........................................................

6. Karama ...........................................................

9.Kuokoka..........................................................

10. Mwisho...........................................................

# 1. MWINJILISTI ?

Mwinjilisti ni mtumishi wa Yesu anayetangaza wokovu uletwao kwa uweza wa mungu au ni mtumishi wa Yesu anayetangaza injili kwa kanisa na watu

Mwinjilisti ni mtumishi wa yesu mwenye huduma ya kanisa ya uinjilisti moja kati ya huduma kuu au kubwa tano za kanisa.

**Waefeso 4:11** "Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa **wainjilisti** na wengine kuwa wachungaji na waalimu;"

Ktk biblia nzima neno Wainjilisti umoja mwinjilisti linapatikana ktk mstari mmoja wa maandiko matakatifu ktk biblia tena ni ktk agano jipya tu.

Twende darasani kidogo tujikumbushe jinsi neno lilivyoundwa au jinsi ya kufafanua neno.

**Wa**injili**sti** :==> Wa + injili + sti

**" Wa "** ni silabi inasimama badala ya nafsi ya mtu ktk wingi yaani wapo zaidi ya mmoja

**"Injili"** ni neno la kati ktk neno mwinjilisti lenye maana kibiblia ni uweza wa mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye.

**Rumi 1:16**

"...**Injili**; ..ni **uweza wa Mungu uuletao wokovu,** kwa kila aaminiye... "

**"sti"** ni ni silabi inasimama badala ya kielezi cha neno **injili.**

Vipo vitabu vinne vya injili vinavyozumzia maisha ya Yesu ktk Biblia navyo Mathayo,Marko,Yohane na Luka. Kwa kuweka msingu mwinjilisti anakiwa kuwa shauku ya kutumiwa na Yesu kutenda yale yote matendo ya uweza wa mungu yaliyoandikwa ktk vitabu vinne vya injili kama kuponywa mwenye homa,kutoa pepo wa kifafa,kubariki watoto kwa kuweka mikono,Kubadili maji kuwa divai n.k

# 2.KUSUDI LA MWINJILISTI

**Kusudi la mwinjililisti** au huduma ya uinjilisti na kuwaletea **wokovu** waliokoka. Mwinjilisti anatangaza wokovu kwa waliokoka lakini anaweza tangaza injili kwa watu..

Huduma ya uinjilisti ina mambo mawili yafuatayo yakuzingatia ktk kutekeleza au kuwajibika ili kufikia kusudi la huduma ambalo ni wokovu wa kila aaminiye yaani waliokoka na wale Baba wa mbinguni amewaridhia kuwapa neema ya kumwamini mungu au Yesu:=.>

**1) Wokovu kwa njia kutendewa matendo makuu mema na mungu**

Mwinjilisti hutumiwa na Yesu kuwatendea matendo makuu mema ya mungu waliokoka kama miujiza,Kuwabariki, Kuwaponya, kuwatajirisha, kuwatoa pepo,kuwafungua waliofungwa ,kuwajaza nguvu za roho mtakatifu, Amani, Furaha, Haki na Upendo .Mwinjilisti ana neema ya kukaa na Kanisa ikiwa atatangaza wokovu badala ya kuhubiri kutubu .

**2)Kutendea watu matendo makuu mema ya mungu.**

Mwinjilisti hutumiwa na Yesu kuwatendea matendo makuu mema ya Mungu watu kama aliyotenda Yesu kwa waisraeli mfano miujiza, Kuwaponya, kuwatoa pepo,kuwafungua waliofungwa .Mwinjilisti ana neema ya kukaa na Kanisa ikiwa atatangaza wokovu badala ya kuhubiri kutubu .Ukweli wa wakati wetu mwinjilisti ukifikia kuwa na mikutano ya injili Yesu atakutumia kuhudumia wenye matatizo yaliyoshindikana kwa wanadamu kama zilivyo huduma zingine za kanisa wakifanya mikutano ya injili mwisho wakati wa karibu na kufunga mkutano wa injili huita watu wa kuokoka ndivyo na mwinjilisti anavyotakiwa kutenda kwa habari ya watu kama zakayo waliopewa wokovu ktk biblia watakutafuta wenyewe kwa wakati wao kama una neema na upako wa kutoka kwa Yesu wa Uinjilisti. Mwinjilisti una kibali pia cha kusimama mbele ya wenye dhambi na kuwatangazia injili.au wokovu Ktk mikutano ya injili.

# 3. KANISA

Mwinjilisti hutumiwa na Yesu kuwapatia wokovu waliookoka yaani kanisa.Yesu humtumia mwinjilisti kuwatendea matendo makuu mema kama miujiza, uponyaji,kubariki,kutoa pepo na kutajirisha,kuwajaza roho mtakatifu na kuwafungua walio-fungwa.

Waliookoka waotendewa hayo pengine kila jumapili wakusa-nyikapo mabadiliko ya maisha yao ni kwa nguvu za mungu hata wao hukiri ni mungu au Yesu ndiye amewatendea.

Mwinjilisti angeliwaza kila kitu kinawezekana kwa nguvu au uweza wa mungu yale ambayo mtu aliyeokoka anaona haya-wezekani kwake sio kwa Yesu.

Wazo la mwinjilisti kukaa au kuwa na kanisa linaoneka ni geni kwa wakati wetu kama ilivyozoeleka miaka ya nyuma ktk ka-nisa (2000 kurudi nyuma) mwinjilisti ni mtumishi wa kutafuta watu wa kuokoka au kufanya mikutano ya injili na kuvuna watu wa kuokoka.

Ni roho mtakatifu kwa kinywa cha mtume,mwalimu na mhubiri .Paulo aliandika huduma mbili zinakaribia kufafanana nazo ni mwinjilisti na mhubiri.

mtume,mwalimu na mhubiri Paulo alitumia huduma ya mhubiri kutafuta wenye dhambi wataokoka kwa kuwahubiria injili na kati miaka 2000 kurudi nyuma kanisa hutumia hudu-ma ya mwinjilisti kufafuta wenye dhambi wataomwamini yesu ni mwokozi na kuokoka.

Niimeandika haya ili **mwinjilisti** apate ufahamu huduma yake inaruhusu kuhudumia **kanisa** lipate **wokovu** na kuwatangazia injili **wenye dhambi** wapate **wokovu** kwa **kuokoka.**

# 4. WENYE DHAMBI (MATAIFA)

Mwinjilisti hutumiwa na Yesu kuwatangazia injili **wenye dhambi** wapate **wokovu** kwa **kuokoka.**

Yesu humtumia mwinjilisti kuwatendea matendo makuu mema kama miujiza, uponyaji,kutoa pepo na kuwafungua waliofungwa.

Neema ya mwinjilisti inawavuta watu matajiri waliopata utajiri wao kwa njia mbovu (rushwa,dhuluma,ujambazi,uuzaji wa madawa kulevya) kama Zakayo kukutafuta mwinjilisti kutubu kwa matendo kupokea wokovu kwa wakati wetu watakutafuta na kuokoka kisha kuopokea wokovu kwa kutoa nusu ya mali yao na kuchangia injili kama tunda la tendo lake la kwanza la toba.

**Luka 19 : 1 –10**

"Naye alipoingia Yeriko alipita katikati yake. Na tazama, palikuwa na mtu, jina lake **Zakayo,** mkubwa mmoja katika watoza ushuru, naye ni **tajiri**. Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, asiweze kwa sababu ya umati wa watu, maana ni mfupi wa kimo. Akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa kuwa atakuja kuipitia njia ile. Na Yesu, alipofika mahali pale, alitazama juu, akamwambia, Zakayo, shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako. Akafanya haraka, akashuka, akamkaribisha kwa furaha. Hata watu walipoona, walinung'unika wote, wakisema, Ameingia kukaa kwa mtu mwenye dhambi. Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, Tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimenyang'anya mtu kitu kwa hila namrudishia mara nne. Yesu akamwambia, Leo **wokovu** umefika nyumbani humu, kwa sababu huyu naye ni mwana wa Ibrahimu. Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. "

# 4.WOKOVU

**Wokovu** ni maisha ya mtu aliyeokoka kama matokeo ya kutendewa mema na mungu mfano miujiza,uponyaji,kutolewa pepo au kufunguliwa,kubarikiwa,kutajirishwa,kupewa ulinzi wa malaika , kujazwa furaha,Amani,Haki and Upendo.

Wokovu kwa waliokoka uletwa kwao na kudhihirika ktk maisha ya kila siku kutokana yupo chini ya huduma ipi ya kanisa pia na huduma iliyo ndani yako au karama unapochochea au kuitumia kupenda kanisa kama Yesu alivyoamuru yaani kuitumia kuhudumia wenzako waliokoka. Wokovu kwa kanisa hupatikana kwa njia zifuatazo:=>

1) Kumkiri Yesu kila siku — wokovu wa aina hii unaupata chini ya huduma ya kinabii maana unayakiri mema ya kesho yako ktk jina la Yesu na yanakuwa kwa kuwa una thawabu wa kinabii na ni mtoto wa kinabii

**Rumi 10:10** "Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata **wokovu.** "

2)Kufundishwa ya Yesu na Baba yake na kuyatenda — wokovu wa aina hii unaupata chini ya huduma ya Mwalimu wa kanisa.Unapofundishwa kuyashika aliyosema Yesu na kuyatenda kwa bidii ndipo matendo yako yatabadilika na kuwa na nuru utazidi kutakasika.

3) Kutendewa na mungu mambo makuu mema kama kutolewa pepo , uponyaji, Miujiza, kubarikwa na kutajirishwa.— **Wokovu** wa aina hii unaupata chini ya huduma ya **Mwinjilisti** wa kanisa au Mtenda miujiza na mponyaji kwa sehemu fulani.

4)Kundishwa na kutendewa ishara na Miujza —- Wokovu wa aina hii unaupata chini ya huduma ya Mtume wa kanisa aliyetumwa na Yesu.

# 5. KARAMA

Ukweli mwinjilisti anapewa roho ya uweza wa mungu kwa kipimo cha Yesu kristo  na roho ya ushauri akiomba au ziada kutoka kwa mungu.

Zifuatazo ni karama za roho mtakatifu zenye uweza wa mungu ndani yake ambazo roho mtakatifu anaweza kumpa mwijilisti kama za vitendea kazi ktk huduma ya uinjilisti ya kanisa iliyo ndani yake:=>

1) Imani ktk roho mtakatifu

2) Uponyaji

3) Miujiza

4) Matendo ya miujiza

Pia Mungu huweza humkirimia mwinjilisti sehemu  zingine za uweza wake zenye kudhirisha nguvu zake kama:=>

1) Amri ya kutoa pepo

2) Kubariki

3) Kutajirisha.

Mungu huweza kumkirimia yote mwinjilisti niliyoandika ili Yesu amtumie kuwapatia wokovu  kanisa yaani waliookoka na kuwadumia wenye matatizo(wagonjwa,pepo,vipofu,bubu) kama Yesu.

Uinjilisti ni  huduma ya kanisa inayotelewa na Bwana Yesu . Bwana Yesu ndiye atoaye na kusimamia huduma za kanisa hasa zile kubwa tano na huduma ya uinjilisti ikiwemo.

**Waefeso 4:11**

“Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa **wainjilisti** na wengine kuwa wachungaji na waali-

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka  kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034